

## **Mchango wa Kiswahili Katika Maendeleo Nchini Kenya**

Dr. Vifu Makoti, PhD,  
Senior Lecturer, Department of Linguistics and Languages,  
Machakos University,  
P.O. BOX 136-90100, MACHAKOS, KENYA.

### **ABSTRACT**

Makala hii itatathmini umuhimu wa lugha (Kiswahili) katika kuchangia maendeleo nchini Kenya. Lugha ni chombo muhimu kwa mwanadamu katika maisha yake ya kila siku. Bila lugha mwanadamu hangekamilika kimaisha. Na lugha ndio msingi wa maendeleo ya mwanadamu. Mwanadamu alianza uzalishaji mali baada ya kuunda lugha. Uzalishaji mali ndicho chanzo cha maendeleo ya mwanadamu. Maendeleo yamejelezwa na wataalamu mbalimbali. Chambers (1997) ameeleza ‘maendeleo’ kwa usahili kabisa kuwa ni ‘mabadiliko mazuri’ (nchini au duniani). Alan Thomas (2000) ameyaeleza kama kuboreka kwa hali ya maisha, afya na maisha bora kwa wote na mafanikio ambayo huleta uzuri wa maisha kwa jamii yote. Haya hutokea kwa awamu ya muda mrefu. Maendeleo kwa jumla humaanisha mabadiliko chanya ya mwanadamu katika harakati zake zote za kimaisha. Je, maendeleo haya mwanadamu atayapataje? Maendeleo ni lazima kwa mwanadamu duniani. Hakuna wanadamu wanaobaki kama walivyo miaka nenda miaka rudi. Kuna maendeleo ya kibinafsi na ya kijamii. Yote haya huwezesha na kiwango bora cha uchumi. Uchumi hukua kutokana na uzalishaji mali. Uzalishaji mali hutokea katika mashamba na mitambo au viwanda. Uwezo huu huletwa na jamii kujifunza mbinu na stadi za uzalishaji mali. Mtu anapojifunza stadi fulani, lazima atumie lugha, lugha anayoiwelewa. Kwa hivyo, stadi haziletwi na Kiingereza bali lugha yoyote ile. Nchi nyingi ulimwenguni hazitumii Kiingereza na zimeendelea sana, mfano Ujarumani, Ufaransa, Italy, Malasyia, Korea Kisini na kadhalika. Kwa hivyo, natujiulize, je, hapa Kenya tunaweza kutumia Kiswahili kujifunza mbinu na stadi mbali mbali za kuzalisha mali? Hii ni kwa sababu Kiswahili ni somo la lazima nchini kutoka shule za msingi hadi shule za sekondari. Aidha ni lugha rasmi na ya taifa. Hivyo ni *lingua franca* nchini. Katika makala hii ninajaribu kudadisi swala hili la Kiswahili kutumika katika uzalishaji mali zaidi kukuza maendeleo, na kutoa mifano kadhaa iliyopatikana nchini Kenya.

**Maneno makuu:** Maendeleo, Uchumi, Uzalishaji Mali, Stadi, Mawasiliano, Lugha

mobile: 0775 095 902/0796 277 565

email: vifusaidi@gmail.com